Meneja wa Mradi wa Elimu Jumuishi Tanzania wa Kanisa la FPCT, Ibrahim Suleiman, akizungumza kwenye warsha ya mgawanyo wa majukumu kwa kamati mbalimbali, zikiwamo baraza la watoto, kikundi cha wazazi na wadau wa elimu jumuishi kutoka wilaya ya Bahi na Jiji la Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

NIPASHE UK 15.

# Watumishi sekta ya uvuvi wafundwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka watumishi wa sekta ya uvuvi kufanya kazi kwa uadilifu, uaminifu na nidhamu ili kuleta tija katika sekta hiyo.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi Sekta ya Uvuvi.

"Viongozi wa ngazi zote tunatakiwa kusimamia na kuchukua hatua, inapotokea mambo ya kinidhamu ya watumishi na watendaji wanapokuwa yameenda sivyo lazima viongozi wa ngazi ya idara, taasisi, kitengo, wizara lazima tusimamie ipasavyo," alisema.

Alihimiza baraza hilo kusimamia ushirikishwaji wa watumishi katika utendaji kazi wa kila siku ili kupunguza manung'uniko.

"Ningependa kusisitiza juu ya umuhimu wa ushirikishwaji wa watumishi katika ufanyaji kazi katika vitengo vyote, sisi wote tunajua ushirikishwaji ni jambo la msingi mahali pa kazi, hasa kwenye mambo yanayohusiana na hizo idara na taasisi na vitengo vyetu tukiwashirikisha wafanyakazi tutapunguza manung'uniko," alisema.

Aliongeza: "Maana kama kuna jambo kubwa tunaliamua tunalipitisha, basi wakati wa utekelezaji hatulaumiani sana kwa sababu wote tumehusika na tumeshirikishwa."

Aliwataka viongozi wa baraza hilo kusimamia nidhamu pamoja na kuchukua hatua pindi yanapotokea mambo ya ukosefu wa nidhamu mahala pa kazi.

"Niwaombe sana ndugu wajumbe masuala ya uadilifu, uaminifu, nidhamu kazini ni masuala ya msingi sana uzuri ni kwamba kuna sheria na taratibu na kanuni zinazotuongoza katika mambo haya, kwa hiyo tunapaswa kuziangalia na kuziheshimu ili kwamba tuweze kutoa huduma kwa wananchi wakati kwa kadri tunavyotegemewa.

"Mimi pia kama waziri ambaye nasimamia shughuli za uendeshaji na utendaji kazi wa kila siku wa wizara haitoshi tu kwamba mimi sihusiki na masuala ya kinidhamu ya kimaadili na uadilifu lakini natakiwa kuhakikisha kwamba wizara kwa ujumla inaendana na masuala ya nidhamu kazini inaendana na masuala ya uadilifu na uaminifu kazini," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Katibu Mkuu anayeshughulikia uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema kikao hicho kitakuwa na agenda za wajibu wa mwajiri na taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na mpango wa bajeti kwa mwaka 2021/22.

Scanned with CamScanner

# *Wafugaji waomba uwekezaji usindikaji mazao ya mifugo

Na Abela Msikula, Mwanza

WAFUGAJI katika Wilaya ya Misungwi wameiomba serikali na wadau wengine kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, kutokana na uwepo wa malighafi za kutosha kulisha viwanda hivyo.

Waliliambia HabariLEO jana kuwa uhakika wa malighafi unatokana na wao kujifunza teknolojia ya kutumia madume bora ya ng'ombe aina ya 'Ankole' na 'Mpwapwa'hatua inayoongeza mazao ya mifugo kama vile maziwa, nyama na ngozi bora.

Walisema teknolojia hiyo imekua ikisambazwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), ambayo imekua ikitoa mbegu za madume ya ng'ombe hao katika kanda.

Mfugaji Maige Shija alisema matokeo ya mchanganyiko wa mbegu za madume hayo na majike ya asili huleta aina ya ndama wenye uzito wa kuridhisha, wanaokuwa na kupevuka kwa haraka.

"Ng'ombe jike anayetokana na mchanganyiko huo wa mbegu huzaa akiwa na umri wa miaka miwili, lakini wa asili humchukua hadi miaka mitatu. Wepesi huu wa kuzaa ni mojawapo ya uhakika wa upatikanaji wa malighafi za kutosha kulisha viwanda kwani wanyama wanakuwa na kuzaliana kwa muda unaotakiwa," alisema.

Kwa mujibu wa Shija, ng'ombe aliyeboreshwa mwenye umri wa mwaka mmoja huuzwa kwa Sh 800,000 ikilinganishwa na Sh 300,000 ya yule wa asili lakini umri uleule.

Mfugaji mwingine, Roberth John alisema TALIRI imekua ikiwafundisha pia namna bora ya kulisha mifugo yao, hali ambayo huongeza maziwa kutoka lita mbili ya ng'ombe wa asili hadi lita sita mpaka nane kwa ng'ombe chotara.

"Faida kubwa kwetu ni upatikananji wa mifugo inayokua haraka na nyama nyingi kutokana na ufugaji huu mpya. Ng'ombe chotara anafikisha takribani kilo120 kwa muda wa mwaka mmoja ikilinganishwa na kilo 70 za yule wa asili. Hata muonekano wa ng'ombe aliyeboreshwa huwavutia wateja mnadani na hivyo kuongeza kasi ya mauzo na manunuzi," alisema.

Mtafiti Msaidizi wa TALIRI katika kitengo cha Wanyama, Nelson Felician alisema takribani madume 55 yameshasambazwa wilayani humo na nje ya wilaya toka mwaka 2012, wafugaji wamekuwa wakisistizwa kuzingatia uwiano wa matumizi ya dume kwa majike ili kupata uzalianaji mzuri na ndama bora.

Alisema uwiano ni dume mmoja kupanda majike 25 kwa msimu wa kupandishwa "Lakini pia inabidi dume kuhamishwa baada ya miaka miwili ili kuepuka kuwazalisha watoto wake na hivyo kuharibu kizazi cha ng'ombe."

Scanned with CamScanner



KUTOKA BUNGENI

NA HAPPINESS MTWEVE, DODOMA

**Ushauri>> Wabunge toeni ushirikiano kuwaelimisha w**

UHURU UK 5.

# Wafugaji wadaiwa kukaidi amri ya kutoingia hifadhini

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amesema baadhi ya wafugaji wa Kijiji cha Buger, wamekuwa na tabia ya kukataa kutii sheria bila shuruti wanapoingiza mifugo hifadhini.

Mary, alitoa kauli hiyo Bungeni, jana, jijini Dodoma, wakati akijibu swali la Mbunge wa Karatu, Daniel Awack (CCM), aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa wananchi wa Buger na Hifadhi ya Manyara.

Akijibu swali hilo, Mary alisema licha ya wafugaji hao kukataa kutii sheria, wamekuwa wakipiga mayowe yanayoashiria hatari kwa mujibu wa utaratibu wa kabila la Wairak.

"Baada ya yowe hilo kupigwa, wananchi hupata morali na hujitokeza wakiwa na silaha za jadi, zikiwemo fimbo, mishale, mapanga na mikuki ili kupinga ukamataji huo wa mifugo, ambapo huchukua mifugo yao kwa kutumia nguvu.

"Kumekuwepo na baadhi ya matukio ya askari kunyang'anywa silaha au mifugo iliyokamatwa hifadhini, hali hiyo husababisha kutokuelewana baina ya askari wa hifadhi na wananchi," alisema.

Aidha, alifafanua kwamba kumekuwepo matukio ya mauaji ya askari wawili huku watatu wakijeruhiwa katika eneo hilo.

Naibu waziri, alisema matukio kama hayo yamekuwa yakijitokeza katika maeneo mengine yanayozunguka hifadhi mbalimbali nchini.

Alieleza kuwa serikali imekuwa ikiunda kamati mbalimbali kuchunguza matukio hayo ili kubaini chanzo cha tatizo.

"Kwa ujumla, imebainika kuwa tatizo kubwa ni wananchi kutoheshimu makubaliano, ambayo yamekuwa yakifanywa mara kwa mara kati ya uongozi wa wilaya, hifadhi, serikali ya kijiji na wananchi, kuhusu taratibu za kufuatwa pindi wao au mifugo inapokamatwa ndani ya hifadhi,»alisema.

Alibainisha kuwa serikali imedhamiria kuleta mahusiano mazuri kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi, kwa kuchukua hatua mbalimbali, zikiwemo kufanya vikao vya kutafuta suluhu pamoja na kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo husika.

Mary, alisema katika kutekeleza azma hiyo, wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itahakiki mpaka wa Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa Kijiji cha Buger.

"Naomba kutoa rai kwa wabunge, kutoa ushirikiano wa dhati katika kuwaelimisha wananchi wanaopakana katika maeneo yaliyohifadhiwa, kuepuka uvunjifu wa sheria za nchi," alieleza.

MAKADIRIO

Scanned with CamScanner

yaliyofanyika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. Kulia ni Naibu Waziri wa Elimu,Sayansina Teknolojia Omari Kipanga. Picha na Deus Mhagale.

wakati wa kipindi cha mapumziko cha bunge jijini Dodoma jana. Kushoto ni Sophia Mwakagenda na Felista Njau.PICHA NA DEUS MHAGALE



TANZANIE UK 21

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi Sekta ya Uvuvi wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa mkutano wa siku moja wa baraza hilo uliofanyika jijini Dodoma, ambapo ulifunguliwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki na kufungwa na Naibu WaziriPg1 Abdallah Ulega. (Picha na Edward Kondela, Afisa Habari ñ Wizara ya Mifugo na Uvuvi)

Scanned with CamScanner